Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tatu - Tarehe 5 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the Year ended 30th June, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 31

**Maisha ya Chini ya Mtanzania**

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA (k.n.y. MHE. SEMINDU K. PAWA)** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutaja mambo makuu machache ambayo imekusudiwa kuyafanya kwa ajili ya kumwinua Mtanzania kutoka katika hali ya chini (duni) ya kimaisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mambo makuu machache ambayo Serikali imekusudia kuyafanya kwa ajili ya kumuinua Mtanzania kutoka katika hali ya chini (duni) ya kimaisha ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni utekelezaji wa Sera ya Kuondoa Umaskini. Serikali itaendelea kutekeleza na kuboresha sera na mipango yenye lengo la kuondoa umaskini hususani katika sekta za kilimo, barabara, afya, elimu na maji hali kadhalika kuboresha huduma katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pili, uimarishaji wa Sekta ya Kilimo. Serikali itaendelea kuimarisha zaidi sekta ya kilimo kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa mkakati wa kuondoa umaskini. Hatua zilizochukuliwa katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya. Fedha hizo zitapelekwa moja kwa moja kwenye Akaunti za Idara za Kilimo za Halmashauri husika ili zitumike kuhudumia zao moja la biashara na moja la chakula.

Aidha, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufidia gharama za usafirishaji wa pembejeo muhimu hasa Mbolea na kutimiza uzalishaji wa chakula ili tujitegemee kwa chakula.

Tatu, udhamini wa mikopo kwa ajili ya shughuli ndogo ndogo kupitia Bajeti ya mwaka 2003/2004 kwa ajili ya kudhamini mikopo ya sekta ya wenye shughuli ndogo ndogo za kibiashara, Mfuko huu utasimamiwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo.

Nne, kujenga Utamaduni wa kuweka Akiba kupitia Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS).* Vyama hivyo vimepata mafanikio makubwa sana na vimewakomboa wananchi wengi walio wanachama.

Mheshimiwa Spika, tano, uwezeshwaji wa wananchi katika uwekezaji mpya kupitia *TIC* kwa kupunguza viwango vya uwekezaji kwa Watanzania wanaoonyesha nia ya kutaka kuwekeza, kiwango cha chini kikiwa dola za Marekani 100,000 kwa Watanzania ikilinganishwa na dola za Marekani 300,000 kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Kwenye Sera ya Madini ya mwaka 1998, Serikali imeandaa utaratibu ambao utawawezesha wawekezaji wadogo kwa kuwapatia mafunzo, kuwasaidia katika kupata vifaa bora na masoko, kukuza uhusiano kati ya wawekezaji Watanzania na wawekezaji wageni na kurahisisha upatikanaji wa leseni.

Sita sera ya *Small and Medium Enterprises* ya Wizara ya Viwanda na Biashara pia inatoa motisha kwa wananchi, kuwasaidia kupata mitaji na mafunzo, uwezeshaji wa kupata teknolojia ya kisasa, utafutaji wa masoko ya bidhaa zao na kuhimiza ufanisi na ubora wa bidhaa ili waweze kushindana na soko la nje.

Mheshimiwa Spika, nguvukazi na ajira, matokeo ya utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2000/2001 yanabainisha kuwa sekta ya kilimo, sekta isiyo rasmi na sekta binafsi ndizo zinazoajiri watu wengi zaidi. Hivyo juhudi za Serikali zitaendelea kulenga katika kuboresha kilimo na kuwezesha uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ili kuyaongezea thamani.

Aidha, vyuo vya majaribio ya ufundi vitahimizwa kutoa mafunzo yanayohitajika katika soko la ajira. Aidha, Serikali itaendelea kutoa motisha kwa viwanda ambavyo vina fursa kubwa ya kuajiri watu wengi kwa mfano viwanda vya nguo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kusema kwamba changamoto iliyoko mbele yetu katika suala zima la kupunguza umaskini ni kuwezesha kila Wilaya kutayarisha na kutekeleza mpango wa muda wa kati wa Wilaya wa kupunguza umaskini na kuhimiza katika ngazi zote kila mtu mzima mwenye uwezo, afanye kazi ili tuweze kupunguza umaskini wa kipato.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza ni kweli kwamba eneo muhimu sana ambalo anatakiwa kusaidia katika kuondoa umaskini ni kilimo, nini mpango wa Serikali wa makusudi kabisa wa kuwa na maduka ya pembejeo ngazi ya Mkoa ili iwe rahisi kupata majembe, mbolea na kadhalika?

Pili, wachimbaji wadogo wadogo wanafanya kazi kubwa sana lakini hawana msaada wowote, nini tamko la Mheshimiwa Waziri juu ya kuwapendelea wachimbaji wadogo wa madini kupata mkopo katika Benki za Wilayani na Mkoani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Kapteni Theodos Kasapira kwamba ni vizuri katika kuboresha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima kuwe na utaratibu wa kuanzisha maduka hasa katika ngazi za Mkoa. Nadhani hili ni suala ambalo litafanyika vizuri zaidi litakapotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Chakula.

Pili, wachimbaji wadogo wa madini wamesaidiwa sana hasa kupitia Sera ya Madini ya mwaka 1998 kwa maana ya kupata mafunzo, kupata vifaa pamoja na utaratibu wa kuruhusu wawekezaji kuleta vifaa hivyo, hivyo vifaa vimekuwa vingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kupata mikopo kwa wachimbaji wadogo ni kama lile linalojitokeza kwa wakulima, wengi wao wanashauriwa waanzishe Vyama vya Ushirika, wajiunge katika vikundi ili waweze kupata mikopo hiyo katika Mabenki wakiwa na dhamana zinazofahamika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua tunatoa dakika tano, tano kwa kila swali dakika tano za swali hili zimekwisha, swali linalofuata!

Na. 32

**Sera ya Serikali ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA (k.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kubinafsisha Mashirika ya Umma:-

(a) Je, ni mashirika ya umma mangapi yamebinafsishwa katika kipindi cha mwaka 1997-2002; na ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutokana na mpango huo na zimetumika namna gani?

(b) Je, ni mashirika ya umma mangapi yanatarajiwa kubinafsishwa katika kipindi cha mwaka 2002-2005 na ni fedha kiasi gani zinatarajiwa kupatikana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 1997 hadi kufikia Desemba, 2002 jumla ya mashirika 99 yalibinafsishwa na kufikia hatua ya mikataba ya mauzo, 26 yalikuwa katika hatua ya makubaliano ya awali na mashirika 29 yalipelekwa *Loan and Advance Realization Trust (LART)* kwa kuuzwa kupitia utaratibu wa ufilisi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mikataba ya Mashirika yaliyobinafsishwa na mali zilizouzwa katika kipindi hicho ni shilingi bilioni 76.6 na dola za Kimarekani milioni 274.3. Jumla ya fedha zilizolipwa na wawekezaji/wanunuzi mbalimbali hadi tarehe 31 Desemba, 2002 ni shilingi bilioni 46.7 na Dola za Kimarekani 109.2

Mheshimiwa Spika, fedha zilizopatikana katika kipindi hicho zimetumika kama ifuatavyo:-

- Madeni ya Mashirika ya Umma ikiwemo malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi na mafao ya wale waliolazimika kuachishwa kazi au kustaafu jumla ya shilingi bilioni 69.5.

- Bajeti ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 80.6.

- Bajeti ya Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 9.2.

- Mfuko wa Ubinafsishaji jumla ya shilingi bilioni 0.9.

(b) Mheshimiwa Spika, Mashirika au Kampuni, vitengo na mali zinazotarajiwa kubinafsishwa katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2004 ni mashirika au kampuni 55 na mali za mashirika 54.

Kuhusu kiasi gani Serikali inatazamia kupata kutokana na ubinafsishaji wa Mashirika/Kampuni hizi, ningependa kusema kwamba si rahisi kutoa takwimu sahihi kwa sababu ubinafsishaji wa mashirika

yote ya Umma hufanywa katika utaratibu wa zabuni. Ni hapo matokeo ya zabuni hizo yatakapofahamika, ndipo tutaweza kujua kiasi cha fedha kitakachopatikana. Bei inakuwa ni kigezo kimojawapo katika kuleta zabuni ambapo mzabuni hupanga bei baada ya kufanya tathmini ya kitaalam kuhusu shirika au kampuni analowania kulinunua. Lakini pia, kuna vigezo vingine vyenye umuhimu mkubwa kiuchumi na kijamii.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Sera hii ya Ubinafsishaji ni Sera ya CCM na ni Sera ambayo imeanza kuonyesha matunda na kwa kuwa moja ya matatizo makubwa yaliyojitokeza katika ubinafsishaji ni matatizo ya ulipaji wa mafao kwa wafanyakazi wa mashirika hayo, je, Serikali inachukua hatua gani kuondokana na kero hiyo ambayo inawapa shida wananchi wetu?

(b) Kwa kuwa kuna mashirika ambayo yamewekwa kwenye kundi la *specified* yameshindwa kuwekeza na kuwa na mipango endelevu ya mashirika hayo ikiwemo Shirika la *TRC,* je, Serikali inasemaje kuhusu mashirika hayo ambayo kwa kweli kwa sababu ya kuwa chini ya mpango huo wa *specified* yameshindwa kuwa na mipango endelevu katika mipango yao ya kila siku?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba moja ya kero katika zoezi la ubinafsishaji ni upatikanaji wa mafao ya wanyakazi hususani mafao yanayoendana na mikataba ya hiari kwa sababu mafao ambayo yanaendana na mafao ya kisheria, Serikali imekwishalipa mafao haya isipokuwa yale yanayoendana na mikatapa ya hiari.

Hata hivyo kama Mheshimiwa Mbunge anavyofahamu sasa hivi Serikali inajaribu kutafuta shilingi bilioni 18 ambazo ni jumla ya mafao yote yanayotakiwa kulipwa kwa wafanyakazi hawa walioachishwa kazi. Mafao haya hayakupatikana kwa sababu wakati ule Mashirika ya Umma yalipokuwa yakiwakata fedha za makato wale wafanyakazi yalikuwa hayawasilishi katika taasisi hizi. Kwa hiyo, mzigo huu umetokana na uzembe na ubadhirifu uliotokea hapo nyuma na ndio maana Serikali imeingilia kati kuona ni jinsi gani inaweza kulipa malipo haya lakini Serikali inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa yale mashirika ambayo ni *specified* kwa mfano *TRC* ni kweli mipango yake endelevu inaanza kulegalega na ndio maana sasa hivi tuko katika mkakati wa kubinafsisha Shirika la *TRC* kupitia njia ya kukodisha. Tayari tumeshalitangaza, tumeshapata wawekezaji kama watatu, watatathminiwa na tuna hakika wakishaingia wale kama wawekezaji binafsi Shirika litaanza kufanya kazi vizuri.

Na. 33

**Wizara Zenye Shughuli za Ki-Muungano**

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa Ki-Katiba zipo Wizara katika Serikali ya Muungano wa Tanzania ambazo shughuli zake ni za ki-Muungano;

Je, kwa nini Mawaziri wa Wizara hizo hawana mpango maalum na unaofahamika wa kufanya kazi Zanzibar japo kwa siku chache kwa mwaka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mikunguni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara zinazoshughulika moja kwa moja na mambo ya Muungano ni pamoja na zile za Mambo ya Ndani ya Nchi, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mbali na Wizara hizo pia kuna Idara na Asasi mbalimbali za Muungano. Hizi ni kama Baraza la Mitihani Tanzania, Mamlaka ya Hali ya Hewa, Usafiri wa Anga, Tume ya Mawasiliano, Bodi ya Biashara za Nje, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, bila kusahau Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara na Asasi zina ofisi zake Tanzania Zanzibar. Viongozi wake wakuu hutembelea ofisi hizo na kufanya shughuli zao kadri wanavyojipangia utekelezaji wa shughuli za kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ofisi yetu inazidi kuwahimiza wakuu wa taasisi hizi kuendeleza shughuli zao Tanzania Zanzibar.

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali ya kumuuliza.

(a) Kwa kuwa bado kuna baadhi ya Taasisi, Asasi nyingine au pengine hata watu matatizo yao hayatatuliki wakati hao wakubwa unaosema wanaopitia kule na wanaokaa kule, je, bado Waziri anaweza kufikiria suala hili la kuwa Mawaziri angalau siku chache waende kufanya kazi kule?

(b) Ikiwa itakuwa hivyo, je, anaweza kutoa ratiba maalum ili watu wajiandae na shughuli zao au kazi zao walizokuwa nazo ili hawa Mawaziri wakienda wapate kazi nyingi za kuweza kufanya wasikae bure kule?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu maoni yake kwamba kuna baadhi ya matatizo hayatatuliki na ingekuwa ni vizuri kufanya kazi kule ikasaidia kutatua matatizo, napenda kusema hivi, Tanzania ni nchi moja uwe na Ofisi Dar es Salaam au Dodoma kama zilivyo baadhi ya Wizara zetu bado kazi za nchi zitafanyika.

Kwa hiyo, suala la ofisi iko wapi na suala la kutimiza wajibu wa ofisi au Wizara inayohusika sioni kama inaathirika kutokana na kwamba ofisi ya Wizara iko Tanzania Zanzibar au iko Tanzania Bara.

Kuhusu ratiba maalum kwamba ingekuwa ni vizuri pengine wananchi wakafahamu, tutaendelea kuwasiliana na wanaohusika pale ambapo inalazimu Waziri mhusika kufanya shughuli zake kama ni Tanzania Zanzibar tuwasiliane na Waziri ambaye anashabihiana na Waziri mhusika katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kusudi wananchi wapate fursa ya kujua kwamba Mheshimiwa Waziri atakuwepo. Lakini pia huwa zipo taratibu za utendaji za kupeana habari kwamba Waziri mhusika atakuwa sehemu gani katika nchi yetu.

Na. 34

**Kero Zinazodhoofisha Muungano**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa yamekuwepo madai kadhaa ndani ya Bunge na nje ya Bunge kwamba zipo kero zinazodhoofisha Muungano wa Jamhuri ya Tanzania:-

(a) Je, Serikali inazijua kero hizo? Kama inazijua izitaje moja baada ya nyingine.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuzipatia ufumbuzi kero hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kutambua matatizo yaliyopo katika utekelezaji wa mambo ya Muungano, tarehe 28 Julai 1992, Serikali iliunda Kamati Maalum iliyokuwa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, ambayo ilichunguza kero za Muungano na kutoa ushauri juu ya namna ya kuzipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo hayo yalihusu masuala ya Uhamiaji, Uraia, Miliki ya fedha za kigeni, ukusanyaji na mgawanyo wa mapato kutokana na kodi ya mapato na ushuru wa forodha, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, misaada, mikopo na msingi wa kuchangia gharama za Muungano, Katiba zetu, Elimu ya Juu, Posta, Simu, Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, Polisi, Bandari, Mambo yanayohusika na usafiri wa anga, Maliasili ya Mafuta na Gesi asilia, Baraza la Mitihani la Taifa na Mahakama ya Rufaa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kupata taarifa ya Kamati Maalum ya Rais ya kushughulikia mambo yanayoleta kero katika shughuli za Muungano, pamoja na taarifa mbalimbali za Serikali ilichukua hatua za dhati ikiwa ni pamoja na kuweka gawio la 4.5% la misaada na mikopo inayotolewa na wafadhili kwa Serikali ya Muungano pamoja na faida ya Benki Kuu kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, sheria mbalimbali zimetungwa na zinatakiwa zitumike pande zote za Muungano:-

Kwa mfano, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sheria ya Uhamiaji, Sheria ya Uraia, Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sheria ya Usalama wa Taifa, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Sheria ya Biashara ya Bima.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafungua akaunti yake Benki Kuu ya Tanzania na Tume ya Pamoja ya Fedha imeshaundwa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo. Aidha, Serikali imekuwa ikitatua kero za Muungano zinazojitokeza kwa kufanya vikao bayana kati ya pande zote za Muungano hata kwa sekta zinazoshughulikia mambo ambayo si ya Muungano.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anayehusika na mambo ya Muungano hakutaja kero moja ambayo ipo na imebainika inahusu mipaka katika Bahari na kwa kuwa mipaka katika Bahari haikuwemo katika *Article of Union* ya mwaka 1964, je, Serikali haioni kuwa ni wakati mzuri sasa kuzungumzia mipaka ya Bahari ikajulikana mpaka wa Zanzibar ni wapi na mpaka wa Tanzania Bara ni wapi ili kuzuia uvuvi haramu unaofanywa na nchi nyingine kwa manufaa ya nchi zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, suala la mipaka ya nchi, tuchukulie kabla ya kupatikana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Tanganyika ilikuwa na mipaka yake inayofahamika Kimataifa na vivyo hivyo Jamhuri ya watu wa Zanzibar ilikuwa na mipaka yake inayofahamika Kimataifa. Sasa baada ya Muungano, mpaka wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulikuja ukajumuisha na ile mipaka ya iliyokuwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, lakini nina hakika anapozungumzia suala la matumizi ya raslimali kama viumbe wa Baharini anazungumzia ule mpaka tunaosema wa Bahari Kuu *(Exclusive Economic Zone)* kwa lugha ya Kiingereza. Sasa ukichukulia hii ambayo wanasema ni kiasi cha kilomita 200 hivi utakuta mpaka huo unazidi ule wa Kijiografia kwa kutambua mipaka ya nchi Kimataifa.

Kwa hiyo, nadhani ni vizuri tukayatofautisha haya mambo mawili, kama tunazungumzia suala la *Economic Exclusive Zone* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sehemu ya Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano inajumuika katika mpaka huo lakini kama ni mipaka iliyokuwa kabla ya Muungano nayo hii Kijiografia inafahamika.

Na. 35

**Sera ya Usimamizi wa Maendeleo ya Miji na Vijiji**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa duniani hakuna kidumucho bila mabadiliko; na kwa kuwa miji yetu na vijiji vyetu vinakua; na kwa kuwa kama Tanzania isipokuwa na sera na usimamizi imara wa maendeleo ya miji na vijiji kuna siku nchi nzima itajaa majengo au nyumba za kuishi hali ambayo itasababisha nchi kupoteza ardhi nzuri kwa kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za uzalishaji mali; na kwa kuwa hali hiyo inatokana na mtindo ulioko nchini wa kujenga nyumba fupi *(bungalow)* badala ya kujenga nyumba za ghorofa ili wakazi wengi waishi katika eneo dogo:-

(a) Kwa kuwa uwezo mdogo wa kiuchumi wa Watanzania wengi waishio mijini unawafanya wapendelee kujenga nyumba fupi na hivyo kupunguza ardhi nzuri ya kilimo, je, kwa nini Serikali kwa kutumia Shirika la Nyumba la Taifa lisijenge nyumba za ghorofa na kupangisha wakazi wa mijini kote nchini ili kuzuia tatizo hilo la ujenzi wa nyumba fupi zinazochukua eneo kubwa zaidi?

(b) Kwa kuendelea kujenga nyumba fupi mijini je, ni lini majengo ya Jiji la Dar es Salaam yataungana na yale ya mji wa Tanga au Morogoro au Moshi au Arusha na kuunda mnyororo mrefu wa miji *(Conurbation)?*

(c) Kwa vile kupanua miji kwa kujenga nyumba fupi kumeambatana na kukua kwa umaskini unaotokana na kuwapokonya wananchi ardhi ya kilimo na kuwahamishia mbali watu wasio na uwezo wa kununua viwanja na kujenga nyumba za kisasa; je, kwa nini Serikali isitumie ushauri huu katika kujenga nyumba za watumishi hapa Dodoma ambapo imeanza kujenga?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Sera ya usimamizi wa maendeleo ya miji na vijiji ipo, ambayo ni Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Sera hii inatekelezwa na Sheria ya Mipango Miji na Vijiji (Sura ya 378) ya mwaka 1956 iliyohuishwa mwaka 1961 na inahuishwa tena kwa kuzingatia matakwa ya sera hii ili kurahisisha utekelezaji wake.

Waheshimiwa Wabunge wote walipewa vijitabu vya Sera hiyo na Watendaji wote wa sekta ya Ardhi na Makazi katika Halmashauri zote nchini wamepewa. Katika Sera hiyo imeelezwa wazi kwamba uendelezaji wa Miji unaweza kufanyika kwa ama kujenga nyumba fupi au nyumba za ghorofa. Kwa kutegemea uwezo kifedha, Shirika la Nyumba la Taifa, mashirika mengine na watu binafsi wanaweza kujenga aina hizo za nyumba kwa kuzingatia mipango iliyoandaliwa katika miji yetu na uwezo wa wateja kumudu gharama za kupanga au kununua nyumba hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Miji utadhibitiwa katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ambayo pamoja na mambo mengine inasisitiza juu ya utumiaji bora wa ardhi mijini (pamoja na kuendeleza miji kwenda juu) na kuweka kikomo cha kusambaa kwa miji.

Aidha, Serikali inaendelea kuandaa na kutekeleza mipango ya muda mrefu na mfupi ya kuongoza ukuaji na uendelezaji wa Miji na Vijiji kwa kuzipanga shughuli zote za matumizi ya ardhi kama vile

kilimo, ufugaji na makazi zifanyike kwa uwiano mzuri na endelevu. Kwa hiyo, hatutarajii mji mmoja kukutana na mji mwingine na kutengeneza mnyororo wa Miji.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini siyo upokonyaji, bali unafanyika kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Mipango Miji zilizopo. Ni muhimu kwa kila makazi wa maeneo yaliyo mjini akaelewa kwamba yuko mjini na kwa hiyo atalazimika kuzingatia masharti ya kuishi mjini. Kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), tukizingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi tutaelewa na kuepuka baadhi ya matatizo ambayo yameelezwa na Mheshimiwa Mbunge na ushauri wake tutauzingatia. Napenda nitumie nafasi hii kumshukuru kwa ushauri wake ambao anautoa mara kwa mara kwa Wizara yangu katika uendelezaji wa miji nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sera na Sheria za usimamizi wa makazi zipo, napenda kutoa wito kwa wananchi, watendaji, taasisi na asasi husika kutoa ushirikiano kwa mamlaka zinazohusika katika kupanga na kusimamia matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini ili kuwa na makazi endelevu nchini.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya hekima ya hali ya juu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Inaelekea sera ipo lakini tatizo ni usimamizi hapa Dodoma hivi sasa kuna nyumba zinajengwa na Serikali, pale Dar es Salaam kuna nyumba zaidi ya 150 zimejengwa na Shirika la JKT na Boko Shirika la *National Housing* inajenga nyumba hizo hizo ni fupi, kule Njombe kutoka mji wa Njombe kuelekea Makete kuna vijiji zaidi ya 17 sasa vimeungana yaani kutoka Njombe, Ramadhani, Wikichi, Ng'anda, Makoga, Kipengele mpaka Molonga je, si vizuri kwa kuzingatia ushauri huo tukaimarisha utekelezaji maana hizi nyumba zinajengwa bila *permit* na kwa njia ambayo kwa kweli watu wanafanya wanavyotaka tusipochukua hatua mapema nchi itaangamia.

Swali ni kwamba si vizuri Wizara ikasimamia utekelezaji wa Sera yake vizuri zaidi?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye tatizo ni usimamizi, sheria, kanuni na miongozo yote ipo na watendaji wote wanayo.

Sasa rai ninayoitoa kwa Waheshimiwa Wabunge wote na viongozi katika Miji yetu yote na katika vikao vyetu ya Halmashauri, maana usimamizi upo kwenye Halmashauri zetu, basi masuala haya tuyasimamie huko na kwenye vikao vyetu watendaji waulizwe na kuhimizwa kuzingatia sheria na miongozo ambayo ipo ili Miji yetu iweze kupangwa vizuri pamoja na Vijiji vyetu vipangwe vizuri ili tuwe na makazi ambayo ni mazuri na endelevu katika sehemu zote za nchi yetu.

Na. 36

**Mabwawa ya Majitaka - *Spencol***

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mabwawa ya maji taka ya *Spencol* yaliyoko kwenye Kata ya Vingunguti, Jimboni Ukonga ni kero kubwa sana ya kiafya kwa wananchi waishio jirani na maeneo hayo yaani wananchi wapatao 50,000 wa Kata za Vingunguti, Buguruni na Tabata:-

Je, ni lini Serikali itayafunga mabwawa hayo ili kuokoa afya za wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabwawa ya Vingunguti yalijengwa na Serikali miaka ya 1970 kwa nia ya kusafisha majitaka kutoka viwandani na nyumba za wakazi walio karibu na mabwawa hayo. Viwanda hivyo ni vile vilivyo kandokando ya Barabara ya Nyerere kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam.

Usanifu wa mabwawa hayo ulilenga katika kuhakikisha kwamba wananchi au viumbe wengine hawapati madhara yoyote. Utaratibu wa viwango vya kumwaga majitaka kwenye mabwawa na baada ya kusafishwa umezingatiwa kwa kufuata Sheria ya Maji Na. 10 ya Mwaka 1981, kifungu cha 8. Hivyo matumizi yaliyokusudiwa ya mabwawa haya ni kusafisha majitaka yanayotoka viwandani na kwenye nyumba za wakazi ili yasiathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililojitokeza ni la ujenzi holela uliofanywa na wananchi kwenye maeneo ya wazi yanayozunguka mabwawa hayo. Wakazi hao walivamia maeneo hayo na kuharibu uzio uliokuwa umejengwa kuyazunguka mabwawa hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mabwawa hayo katika kusafisha majitaka, haitakuwa busara kuyafunga. Kama yatafungwa wananchi na viwanda vinavyotumia mabwawa hayo watakosa kabisa sehemu ya kumwaga na kusafisha majitaka. Hivyo kero inayozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge itaongezeka na kuathiri eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ingawa *DAWASA,* chini ya mradi wa ukarabati wa miundombinu ya *DAWASA,* watayafanyia ukarabati mabwawa haya ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, ufumbuzi wa tatizo hili ni kuhamisha wananchi waliovamia maeneo hayo na kujenga kinyume na taratibu za makazi. Hivyo, ninashauri uongozi wa Jiji, akiwemo Mheshimiwa Mbunge wafanye utaratibu wa kuwatafutia maeneo mengine ya makazi wananchi waliovamia maeneo hayo ya mabwawa.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo ningependa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa bado kuna ukweli kwamba mabwawa hayo kwa harufu inayotoka pale na uchafuzi yanaathiri kwa kiasi kikubwa sana afya za wananchi hawa wapatao hamsini wanaozunguka maeneo hayo. Je, Serikali itakubali kufanya utafiti kuona ni athari gani za kiafya wananchi hawa wamepata na wanaendelea kupata ili kuchukua hatua za kuwasaidia kiafya kwa maana ya kuwapa madawa na mambo kama yale?

Pili, kwa kuwa kazi ya kuhamisha wananchi katika maeneo hayo ambayo ni makubwa ni mradi ambao hata Serikali yenyewe inaogopa kufanya kwa sababu ni vigumu kuutekeleza kwa sababu ya kuachwa kwa muda mrefu. Je, Serikali haioni kwamba hawa watu si rahisi kuhama na njia nzuri ama kuhamisha hayo mabwawa au kuyawekea mazingira ambayo hayatachafua afya za watu kwenye eneo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge kuhamisha wananchi ni gharama, hilo nakubaliana naye, lakini pia kufanya *modification* ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa maeneo hayo, pia nayo ni gharama.

Kwa hiyo, ninachomweleza Mheshimiwa Mbunge kuwahamisha wananchi baada ya kupatiwa viwanja sehemu nyingine kunawezekana, kwa sababu wapo pale kinyume cha sheria za mipango Miji, kwa sababu Miji imegawanywa, kuna sehemu za viwanda, huduma za jamii na kadhalika. Sasa uvamizi uliofanyika moja kwa moja unaathiri huduma ambazo zilitakiwa kutolewa kwa ajili ya viwanda vinavyozunguka eneo hilo. Sasa hata tukihamisha majitaka tuyapeleke sehemu nyingine bado hatutatatua tatizo kwa sababu viwanda sasa hivi vitakosa mahali pa kumwaga uchafu kutoka kwenye uzalishaji wa viwanda hivyo. Kwa hiyo, bado nasisitiza Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na Halmashauri kwa awamu wanaweza kutatua tatizo hilo bila kuathiri mipango miji ambayo imetengenezwa kwa gharama kubwa na Serikali. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekuwa na mtindo wa kuwanyamazia kimya wale wote ambao inawaona wanajenga kiholela kama vile maeneo ya Ukonga, Kongowe na huko Tabata kwenye maji machafu na kwa kuwa ni Serikali ndiyo inawajibika kuwashauri wananchi waelewe hapa panastahili kujengwa au siyo pa kujenga na hivyo kuwafanya wananchi kudidimia katika dimbwi la umaskini baada ya kufukuzwa katika sehemu hizo.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwafikiria hawa ambao imewaacha kwa muda wa miaka mingi wakajizatiti kuwafidia kokote kule ambako wanakwenda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaposema Serikali ina maana ndefu, maana yake kwamba tuna aina karibu nne za Serikali, kuna Serikali za Vijiji, Serikali za Miji au Serikali za Mitaa na Serikali Kuu na katika kutekeleza hilo alilolisema mhusika mkuu ni hizo Serikali mbili yaani Serikali za Vijiji na Mitaa na Serikali inatoa ushauri na sera kama inavyotakiwa.

Kwa hiyo, uvamizi huo uliofanyika, umefanyika *with full knowledge* au kwa kuelewa fika wahusika ambao tungewategemea wasimamie shughuli za mipango Miji ili kukidhi mahitaji ya maisha Mijini. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge tuwe kama tulivyoelezwa na Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwamba tuwe karibu zaidi katika kusimamia badala ya kuja kutatua tatizo la watu ambao walivunja kanuni na sheria. *(Makofi)*

Na. 37

**Matatizo Makubwa ya Maji - Kijiji cha Kineng'ene**

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Kineng'ene kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Lindi kina matatizo makubwa sana ya maji jambo linalowafanya akinana mama wengi kukesha visimani wakisubiri maji na kuwapa usumbufu mkubwa na kwa kuwa Kijiji hicho kipo katika mradi wa *JICA* wa kuchimbiwa visima na milioni moja kama sehemu ya mchango wao kabla ya mradi huo kuanza kutekelezwa na kwa kuwa sasa imepita miaka miwili lakini hakuna chochote kilichofanyika:-

(a) Je, mradi huo unatarajiwa kuanza lini ili kuwaondolea kero wanakijiji na hasa akinamama ambao wanasumbuka sana kutafuta maji?

(b) Kwa kuwa pamoja na kuwepo kwa wahisani wa *JICA* bado wajibu wa Serikali wa kuwapatia wananchi maji uko palepale; je, Serikali kwa kutambua ukweli huo iko tayari kutoa fedha ili kuchimba visima walau vitatu wakati ukingojewa utekelezaji wa mradi wa *JICA?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *JICA* kwa msaada wa Serikali ya Japan ina lengo la kusambaza huduma za maji Vijijini katika Mkoa wa Lindi ili kuwaondolea akina mama matatizo ya kukesha visimani. Vijiji vipatavyo 33 vya Mkoa wa Lindi kikiwemo Kijiji cha Kineng'ene vitachimbiwa visima chini ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tenda za ununuzi wa vipuri vya mitambo ya kuchimbia visima vilivyoko *DDCA* sasa, upatikanaji wa vifaa vipya vya kuchimbia visima pamoja na magari ya kutekelezea mradi huo, zimefunguliwa mwezi Januari mwaka huu. *Tender* hizo

zimechambuliwa na Serikali imekwishaingia Mkataba na Kampuni itakayonunua na kuleta vifaa hivyo. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuanza kuingia hapa nchini mnamo mwezi Juni, 2004 au mpaema zaidi. Utaratibu umepangwa ili mnamo mwezi Juni, 2004 Serikali ya Japan na Serikali ya Tanzania zitaingia makubaliano yatakayowezesha kutangazwa kwa tenda ya kupata Kampuni itakayofanya kazi ya kuchimba visima hivyo.

*Tender* hiyo inatarajiwa kufunguliwa na kuchambuliwa mnamo mwezi Desemba, 2004 ili kampuni itakayochaguliwa kuchimba visima hivyo (pamoja na vingine 31 vya Mkoa wa Mtwara) ianze kazi hiyo mwezi wa Januari, mwaka kesho wakati vifaa vyote vya kutekelezea mradi huo vitakuwa vimefika nchini. Jumla ya shilingi bilioni 3.17 zitatumika mwaka huu 2004 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mitambo. Utekelezaji wa mradi huu utakamilika ifikapo mwaka 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wajibu wa Serikali upo pale pale wa kuwapatia wananchi majisafi na salama na kutokana na sababu hiyo Serikali ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mpango *Regional Integrated Programme Support (RIPS)* na wananchi wa Kineng'ene wamewezesha kufanya utafiti wa maji ya chini ya ardhi.

Maeneo zaidi ya 10 yameonyesha kufaa kuchimbwa visima vifupi. Kutokana na mpango huu visima vinne vyenye pampu za mikono vimechimbwa na vinafanya kazi. Jitihada za kupata fedha za kuchimbia visima zaidi katika maeneo yaliyoonyesha kuwa na maji ya ardhini zinaendelea.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwamba visima vilivyopo sasa hivi vyote havitoi maji na ndiyo nimeleta swali hili kwa malalamiko kwamba maji hakuna kwa sababu ya ukame na visima vifupi havifai kwa pale. Je, Serikali itakuwa tayari kutuchimbia kisima angalau kimoja kirefu wakati huu?

Pili, kipindi cha kutoka sasa mpaka mwaka 2007 ni kipindi kirefu sana, je, Serikali haioni umuhimu kweli wa kuwanusuru wananchi hao na shida ya maji iliyopo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya visima vilivyochimbwa kwenye Wilaya zilizo Mkoani Lindi havina maji kutokana na ama kuharibika kwa visima vyenyewe au kukauka maji na visima hivi vingi vilichimbwa kwa msaada kutoka Finland kwenye miaka ya 70.

Kwa hiyo, kwa kutambua hilo ndiyo maana Serikali ikaomba msaada kutoka Serikali ya Japan ili kujaribu kutatua matatizo kwa nguvu tutakazoweza kufikia ili kupunguza matatizo ya maji katika Wilaya ya Lindi na sehemu nyingine za Kusini ukiwemo Mkoa wa Mtwara.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa vile pia ni mjumbe kwenye Bodi ya Maji ya Wilaya yake au ya Mji wa Lindi na Vijiji hivyo alivyovisema vipo karibu na Mji wa Lindi wajaribu kuangalia taratibu za kutatua tatizo hili kwa muda huu wakati Serikali inajiandaa zaidi kulitatua tatizo hili kwa muda mrefu.

Na. 38

**Nyumba kwa Wapiganaji wa Vikosi vya *14KJ* na *15KJ***

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa wapiganaji wa vikosi vya Jeshi vya *14KJ* na *15KJ* katika Jimbo la Wawi wanalo tatizo kubwa la nyumba za kuishi na kwa kuwa katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004, fedha za ujenzi wa nyumba hizo hazikutengwa:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha za ujenzi wa nyumba hizo katika Bajeti ya mwaka 2004/2005?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa nyumba za makazi ya wapiganaji wetu katika makambi ya Jeshi ni tatizo sugu ambalo Serikali ya Awamu ya Tatu imelivalia njuga. Utatuzi wa tatizo hilo umeandaliwa katika mpango kamambe wa miaka 15 wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wa kukamilisha viporo vyote vya ujenzi wa nyumba makambini na kujenga nyumba mpya kwa kutumia vikosi vya ujenzi vya Jeshi la Kujenga Taifa.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao vikosi vyetu vya Jeshi la Ulinzi viko katika Majimbo yao ya uchaguzi kwa kuwa karibu na majeshi yetu kufuatilia matatizo yao. Moyo huo wa kuwajali wapiganaji wetu umewapa imani, ari na faraja wapiganaji wetu kuwa jamii inajali na kuthamini michango yao ya kutetea na kulinda amani, utulivu, umoja, uhuru na muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu wakati wa kuwasilisha Makisio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mwaka wa fedha 2003/2004 kuwa Serikali imeandaa programu inayolenga kutanzua tatizo la uhaba wa nyumba za makazi jeshini. Lengo ni kukamilisha ujenzi wa viporo vya nyumba 1,111 katika makambi kumi. Nyumba hizi zilianza kujengwa tangu mwaka 1988.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa viporo vya nyumba 90 katika Kambi ya Ihumwa - Dodoma na nyumba 90 katika kambi ya Sofa - Monduli, umekamilika na familia 180 za wapiganaji waliokuwa wanaishi uraiani wamehamia nyumba hizo za kisasa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viporo vya nyumba 831 katika makambi yaliyobaki nane utaanza mwezi Machi, 2004 katika kambi ya Makoko - Musoma na kufuatiwa na makambi ya Makambako, Kibaha, Lugalo, Nguvumali, Kange, Ihale na Mkalama. Ujenzi wa viporo vya nyumba hizo utatekelezwa na kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutumia fedha za Bajeti ya Serikali, Wizara ya Ulinzi inakamilisha majadiliano na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 20 kupitia Wizara ya Fedha. Mkopo huu ukipatikana Jeshi la Kujenga Taifa litaweza kukamilisha ujenzi wa viporo vya nyumba 831 na kuanza ujenzi wa nyumba mpya katika kipindi cha mwaka mmoja.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi kuwa ujenzi wa nyumba za vikosi vya 14KJ na 15KJ vilivyoko Pemba utawekwa katika mpango huu ambao utatekelezwa kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu majibu hayo na naamini Mwenyezi Mungu atamjaalia atatekeleza. Lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza kwa sababu siku zitakuwa za mbele sana najua.

Kutokana na upungufu mkubwa wa nyumba za kuishi katika vikosi hivyo vya *14KJ* na *15KJ* katika Jimbo la Wawi, wapiganaji wengi wanajitahidi hivi sasa kujijengea nyumba zao wenyewe huko uraiani lakini wanapungukiwa na vifaa muhimu vya ujenzi. Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuwakopesha vifaa vya ujenzi askari hao? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa kutokana na uchache wa nyumba za kuishi Jeshini, askari wengi wanaishi sehemu za mbali uraiani na wanatumia usafiri wa kulipia yaani daladala pale wanapowahi kazini na kwa kuwa kufanya hivyo hulazimika kupoteza fedha zao nyingi kuwalipa madreva kila siku. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa posho nzuri au kubwa ya usafiri askari hao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kutambua kwamba jitihada zinafanywa ili wapiganaji wetu wote tuweze kuwarudisha makambini. Mpango huu ni mpango wa muda mrefu miaka kumi na mitano, umegawanyika katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Sasa upungufu wa nyumba kuhusu wapiganaji ambao wamejitolea kujenga nyumba zao binafsi Wizara ya Ulinzi imeandaa utaratibu kuhusu maduka ambayo yapo katika makambi kuhakikisha kwamba maduka hayo yanaleta vifaa vya ujenzi na kuwakopesha wapiganaji kwa bei nafuu na hili tutaanza kulitekeleza kuanzia mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri, ni kweli usafiri ni tatizo kubwa lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la usafiri siyo kwa wanajeshi tu lakini ni tatizo la taasisi zote. Wizara ya Ulinzi ina mpango wa kuhakikisha kwamba usafiri wa anga, usafiri wa majini na usafiri wa nchi kavu unaboreshwa zaidi, kwa sasa tumeshanunua ndege mbili kubwa za kuweza kuchukua wanajeshi 96 kila moja kuwasafirisha bure popote walipo. Tumepata *beach craft,* meli mbili ambazo zinaweza kutua kila mahali, ambazo ni mpya. Tuna mpango wa kununua magari ya usafiri pamoja na mabasi kwa ajili ya wanajeshi wetu na wanajeshi wameshaelewa. *(Makofi)*

Na. 39

**Malipo ya Mafao ya Wastaafu wa JWTZ**

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Wanajeshi wa JWTZ ni miongoni mwa watumishi wa umma kama walivyo watumishi wengine na kwa kuwa askari hao wanapokuwa kazini wanafanya kazi vizuri ya kulinda nchi yetu popote wanapotakiwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria lakini wanapomaliza muda wao wa kazi hawalipwi mafao yao ya pensheni kwa wakati:-

(a) Je, ni askari wangapi ambao hawajalipwa mafao yao ya kustaafu tangu mwaka 2000-2003?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha wanachodai?

(c) Je, mafao ya wanajeshi hao yatalipwa lini?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mafao ya pensheni ya wanajeshi wastaafu ni pamoja na malipo ya asilimia 33 ya mshahara kwa muda wote wa utumishi ambayo hulipwa baada ya kila miezi sita, kiinua mgongo ambacho hutegemea muda wa utumishi na cheo na mshahara aliokuwa analipwa hadi tarehe ya mwisho ya utumishi wake. Pia husafirishiwa mizigo kutoka kikosini hadi alikoamua kuishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha taratibu zote za mstaafu, Mkuu wa Kikosi chake hupeleka faili la mstaafu Makao Makuu ya Jeshi ambapo Bodi ya Pensheni *(Service Pension Board)* ya Makao Makuu ya Jeshi hulipitia faili ili kuhakikisha kuwa taratibu zote zimekamilika. Faili la mstaafu hupelekwa Hazina kwa ajili ya kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kabla ya kuandika hundi na baadaye mhusika kutumiwa hundi kulingana na anuani yake kama ilivyojazwa katika fomu yake ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa tatizo la kutolipa mafao ya pensheni ya wastaafu kwa wakati limekuwapo jeshini kwa muda mrefu, hii imetokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, wakuu wengi wa vikosi walikuwa hawakagui usahihi wa anuani zilizokuwa zinaandikwa na wastaafu, baadhi ya wastaafu walikuwa wanatumia anuani ya Makao Makuu ya Jeshi, wengine walikuwa wanawaagiza ndugu zao au jamaa zao kuwachukulia hundi za mafao yao kinyume na taratibu za malipo. Mwisho, mivutano katika familia kuhusu mirathi kwa mwanajeshi aliyefariki pia imechangia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya mafao, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Hazina itaanzisha utaratibu mpya wa kuwaondolea kero hii wapiganaji wetu na familia zao. Hundi zote za wastaafu zitatumwa na Hazina Makao Makuu ya Jeshi, Idara ya Pensheni ambapo zitahifadhiwa hadi wastaafu watakapoarifiwa kwa maandishi kupitia Serikali za Mitaa, Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Waheshimiwa Wabunge kuja kuchukua hundi zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Idadi ya wanajeshi ambao hawajalipwa mafao yao kuanzia mwaka 2000 - 2003 ni 76 tu, maafisa ni watano na askari 71. Wapiganaji 58 kati yao ni wastaafu wa mwaka 2003. Hundi za malipo zimekamilika kwa askari wote 76. *(Makofi)*

(b) Kiasi cha fedha kinachodaiwa ni shilingi 519,868,688.20. Kiasi ambacho kimekwishalipwa kuanzia mwaka 2000-2003 ni shilingi bilioni 27.67 kati ya shilingi bilioni 28.2 kilichokuwa kinadaiwa.

(c) Mafao ya wanajeshi hao yatalipwa mara wastaafu hao watakapojitokeza Makao Makuu ya Jeshi au kwa kutumia ofisi za Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa vikosi vilivyoko jirani na wanakoishi. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itatuma orodha ya wahusika kwa Wakuu wa Wilaya zote nchini ili wahusika wajulishwe. Kadhalika tunatoa wito kwa familia za wanajeshi waliofariki kukamilisha taratibu za mirathi Mahakamani ili wahusika waweze kulipwa.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Serikali huwa inajua rasmi kuwa kuna wanajeshi watastaafu katika kipindi fulani, sasa je, kwa nini Serikali haitengi fedha makusudi inapofika wakati wa kustaafu askari wakapata mafao yao badala ya kusubiri muda unapofikia? *(Makofi)*

Pili, kuna wanajeshi wengi waliofariki dunia na mpaka hivi ninavyoongea hawajapata mafao yao wakiwemo ndani ya Jimbo langu la Mkanyageni. Je, Serikali inasema nini katika kuwalipa mafao hayo warithi wa marehemu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kulipa mafao umewekwa na Hazina na fedha hizi ni fedha za wananchi na shughuli za fedha ni nyingi huwezi kutenga fedha zikae zikingojea mtu astaafu. Hilo la kwanza.

La pili, lazima tukamilishe taarifa zote muhimu kuhusu wastaafu. Tukifanya hivyo tutajiweka sawa katika usimamizi wa kusimamia fedha. Kwa kuwa mhimili wa malipo ya wastaafu ni Hazina na utaratibu huu umewekwa na Hazina sasa Jeshi la Ulinzi haliwezi kuingilia taratibu ambazo zimewekwa na Hazina. Lakini nataka nimhakikishie kwamba tatizo hili litakwisha kwa sababu Wizara ya Ulinzi imekwishaweka mtandao wa kompyuta vikosini kwa ajili ya kuwa na *database* yenye taarifa muhimu za

kila mpiganaji, kwa hivyo tutajua mapema kabisa mwaka mmoja kabla kwamba nani anastaafu na *data* zake zitakuwepo na usumbufu huu utamalizika.

Kuhusu waliofariki, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuonane naye tuweze kutatua tatizo hilo, hilo ni tatizo la utekelezaji. *(Makofi)*

Na. 40

**Mpango wa Elimu ya Watu Wazima**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1970 na 1980 nchi yetu ilisifika sana Barani Afrika kwa jitihada zake za kufuta ujinga kupitia Mpango wa Elimu ya Watu Wazima; na kwa kuwa Vituo vya Elimu hiyo vilikuwa katika maeneo ya shule za msingi na kwenye Taasisi mbalimbali lakini sasa hivi elimu hiyo haipo tena:-

(a) Je, ni sababu gani zilizosababisha kuondolewa kwa mpango mzima?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuirejesha tena elimu hiyo nchini ili watu wengi zaidi waendelee kufaidika?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Elimu ya Watu Wazima haujaondolewa. Elimu ya Watu Wazima ni miongoni mwa majukumu saba ya Wizara yangu kama ambavyo huwa nayaorodhesha katika hotuba zangu za Bajeti za kila mwaka. Ni kweli kuwa katika miaka ya 1970 na 1980 nchi yetu ilisifika sana Barani Afrika katika jitihada za kufuta ujinga kupitia Mpango wa Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1986 nchi yetu ilifikia asilimia 90.4 ya watu wazima waliojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Lakini hivi sasa imeshuka hadi kufikia asilimia 68 ambayo inaonyesha kuwa asilimia 32 ya Watanzania hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Mafanikio ya miaka ya 70 na 80 yalichangiwa na misaada mingi ya fedha kutoka kwa Wahisani pamoja na mafanikio ya *UPE,* ule Mpango wa *UPE* ambapo uandikishaji katika elimu ya msingi ulifikia kilele cha *GER* ya asilimia 98 mwaka 1980. Utoaji wa elimu ya Watu Wazima umezorota kutokana na sababu tano zifuatazo:-

(i) Wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kuanza kuongezeka tena kutokana na kudidimia uandikishaji katika shule za msingi kutoka kilele cha *GER* ya asilimia 98 mwaka 1980 hadi asilimia 70 mwaka 2000.

(ii) Uhaba wa mafungu ya fedha za kuendeshea Programu za Elimu ya Watu Wazima kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

(iii) Mabadiliko mengi ya kisiasa na kiuchumi duniani kuanzia miaka ya 80 yaliathiri Wahisani waliokuwa wanafadhili utoaji wa elimu hiyo.

(iv) Mitaala na mbinu za ufundishaji watu wazima zilizoshindwa kuwavutia walengwa.

(v) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilijielekeza mno katika kutoa Elimu ya Sekondari kwa watoto kupitia mfumo rasmi na kuacha kushughulikia Elimu ya Watu Wazima kwa mfumo wa utoaji elimu usio rasmi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inachukua hatua mbili zifuatazo kwa lengo la kufufua na kuimarisha mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima hapa nchini:-

(i) Wizara imeandaa mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Watu Wazima wa Elimu ya Mfumo usio Rasmi *(Adult Education Non-Formal Education Strategy)* wenye mipango miwili;

(a) MEMKWA: Mpango wa Elimu Msingi kwa walioikosa kwa ajili ya watoto wa miaka 11 - 14 na vijana wa miaka 15 - 18 kwa *syllabus* tofauti.

(b) MUKEJA yaani Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii unaowalenga watu wazima kwa mtindo shirikishi wa riflekti.

(ii) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeelekezwa kuacha kujishughulisha na utoaji wa elimu ya sekondari kwa watoto kupitia mfumo rasmi wa zilizoitwa Sekondari za Elimu ya Watu Wazima, badala yake irudi kwenye jukumu lake la kutoa elimu ya kawaida na mafunzo kwa watu wazima kupitia mfumo usio rasmi *(Non-formal Education).* Taasisi hiyo inatakiwa itoe mafunzo kwa walimu wa elimu ya watu wazima na mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu kwa wananchi kwa mtindo shirikishi wa *reflect* unaozingatia mambo wanayopenda kujifunza katika maeneo yao wanayoishi au kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo mbili tunaendelea kuliziba bomba linalotoa watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kufanikisha uandikishaji darasa la kwanza wa watoto wote wa miaka 7 wa kila mwaka na kuhakikisha wanabakia shuleni mpaka wahitimu darasa la saba.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa mipango yake ya kufuta ujinga nchini.

La kwanza, kwa kuwa mpango ule wa zamani haukuwa na gharama kama inavyodhaniwa kwa vile walimu na watumishi mbalimbali walitumika mahali pale walipo. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vizuri angetumia mpango ule ule wa zamani ambao walimu walitumiwa na ndiyo maana tulikuwa na Waratibu Elimu Kata wa kusimamia elimu hiyo?

La pili, inaonekana haijafutwa elimu ya watu wazima. Lakini mimi ningetaka kuona darasa la elimu ya watu wazima, je, naweza nikalikuta wapi kwa sababu mimi kwenye Jimbo langu silioni? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba ule mpango wa zamani tuliokuwa nao wa kuwatumia walimu katika shule za msingi na pia waratibu ulikuwa unaendeshwa kwa gharama nafuu. Lakini napenda niseme kwamba pamoja na kwamba ulikuwa unaendeshwa kwa gharama nafuu tumeiona hali hiyo ya kudidimia kwa elimu ya watu wazima. Mpaka imefikia anauliza swali la pili, kwamba akitaka kuwaona wanafunzi wa elimu ya watu wazima anawakuta wapi?

Mimi nakubaliana naye kwamba mara nyingi tunaalikwa kwenye sherehe za Elimu ya Watu Wazima za kila mwaka. Lakini tumefikia mahali ambapo mtoaji wa taarifa na wewe Mheshimiwa Mbunge uliyealikwa kuwa mgeni wa heshima wote mnaelewa kwamba yanayosemwa mle hayana usahihi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napenda tukiri kabisa kwamba jambo hili lilififia. Katika mipango ile miwili niliyoieleza ndiyo hatua za kutaka kufufua elimu ya watu wazima kwa uhakika. *(Makofi)*

Lakini la kwanza kabisa basi kwa vile sasa tuna shule ya msingi katika kila kijiji basi lile bomba linalowatoa wale wasiojua kusoma na kuandika tujitahidi kuliziba kwa watoto wetu wote kujiunga na elimu ya msingi kwa umri unaotakiwa na wahitimu mpaka darasa la saba.

Halafu elimu ya watu wazima ianze kuwashughulikia wale ambao hawakuwa wameipata katika utaratibu wa yale mambo mawili. Tutakapoanza mpango huo ninahakika tutaanza kuyaona tena yale madarasa ya elimu ya watu wazima. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kufifia kwa mpango ule kulichangiwa kwa kuwaacha walimu bila kuwapa motisha, ndiyo kumechangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa suala zima la elimu ya watu wazima nchini; na kwamba kama Wizara itakuwa imelitazama hilo na kuwapa motisha walimu kutachangia kwa kiasi kikubwa sana kufufua suala zima la elimu ya watu wazima nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kutokana na ufinyu wa Bajeti ambao nimekiri katika jibu langu la msingi, masuala ya ulipaji wa motisha yalizidi kudidimia na watu walipojikuta kwamba hawalipwi basi walianza kupuuza kuifanya kazi hiyo. Katika mipango hii miwili niliyoisema MEMKWA na MUKEJA, ulipaji wa motisha zinazohitajika utazingatiwa. Tunatengeneza Bajeti kamili na sasa hivi semina zinaendeshwa kwa ajili ya uwezeshaji wa ngazi ya MEMKWA na mpango umeandaliwa na kupangiwa fedha ili wale watakaoshiriki waweze kupewa malipo yanayohitajika. *(Makofi)*

Na. 41

**Elimu ya Sekondari**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni ukweli kwamba uwekezaji katika sekta ya elimu una tija zaidi Kitaifa na kwamba ni kweli ukitaka kuua utaifa na nchi yoyote ni kuhujumu mpango wao wa elimu; na kwa kuwa elimu ya Sekondari ni kiungo kimojawapo katika mfumo mzima wa elimu Kitaifa;

Je, Tanzania ina shule ngapi za Sekondari na ziko ngapi kwa kila Mkoa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uwekezaji katika sekta ya elimu unayo tija kubwa Kitaifa, ndiyo maana kwa msingi huo, Wizara yangu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 inahimiza uboreshaji, upanuaji na utoaji wa elimu kwa usawa. Ili kufikia malengo hayo Serikali imebuni programu ya maendeleo ya Sekta ya Elimu yaani *Education Sector Development Programme* kwa kifupi *ESDP* kuwa lengo la kupanua, kuboresha na kuimarisha usimamiaji wa elimu na mafunzo kwa madhumuni ya kuongeza tija.

Katika utekelezaji wa programu hiyo, Serikali iliamua kwa makusudi kuanza na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) wa miaka 5 kuanzia 2002 hadi 2006 wenye lengo la kuboresha, kupanua na kuimarisha usimamiaji wa elimu ya msingi. Katika hatua ya pili, Serikali kupitia Wizara yangu imekamilisha kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) wa miaka mitano kuanzia 2004 - 2009, kwa lengo la kuimarisha usimamiaji, uboreshaji na upanuaji wa elimu ya Sekondari iwafikie asilimia 50 ya rika lengwa la miaka 14 - 17 kwa K1 - K4; na asilimia 25 ya rika lengwa la miaka 18 - 19 kwa K5 na K6.

Hivi sasa Tanzania Bara ina jumla ya shule za sekondari 1,143, kati ya hizo 689 ni shule za Serikali na 454 ni shule zisizo za Serikali na Kimkoa hadi kufikia Desemba, 2003 ilikuwa kama ifuatavyo:-

| Mkoa | Idadi ya Shule | Shule za Serikali | Zisizo za Serikali |
|---|---|---|---|
| Arusha | 67 | 40 | 27 |
| Dar es Salaam | 68 | 14 | 54 |
| Pwani | 31 | 19 | 12 |
| Dodoma | 46 | 33 | 13 |
| Iringa | 69 | 40 | 29 |
| Kagera | 61 | 45 | 16 |
| Kigoma | 27 | 18 | 9 |
| Kilimanjaro | 149 | 67 | 82 |
| Lindi | 18 | 13 | 3 |
| Manyara | 35 | 29 | 6 |
| Mara | 53 | 39 | 14 |
| Mbeya | 77 | 38 | 39 |
| Morogoro | 49 | 30 | 19 |
| Mtwara | 25 | 21 | 4 |
| Mwanza | 58 | 40 | 18 |
| Rukwa | 28 | 20 | 8 |
| Ruvuma | 40 | 25 | 15 |
| Shinyanga | 41 | 29 | 12 |
| Singida | 33 | 23 | 10 |
| Tabora | 35 | 21 | 14 |
| Tanga | 71 | 42 | 29 |

Mheshimiwa Spika, shule za Serikali mwaka huu bila kupanuliwa zinao uwezo wa kusajili kidato cha kwanza wanafunzi 58,159 ambao ni sawa na asilimia 13.1 ya watoto wote waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2003 na ni asilimia 29.6 ya watahiniwa 196,273 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2003.

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda mwuliza swali la msingi peke yake atapata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Lakini pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza nataka niyaulize nipatiwe ufafanuzi.

(a) Kwa vile kwenye majibu yake ya swali la msingi kunadhihirika uwiano usiolingana baina ya Mikoa hiyo hasa kwa idadi ya shule zilizotajwa na kwa vile mipango hii miwili aliyoitaja Mheshimiwa Waziri ya *SEDP* na *PEDP* inalenga kuendeleza na kuboresha shule zile zilizopo tu hazijengwi shule mpya. Serikali sasa ina mpango gani wa kuhuisha kasi ya maendeleo ya sekta hii ya elimu ya sekondari katika Wilaya zile ambazo sasa hivi zinadhihirika kwamba ni *underserved* kama vile Tandahimba? *(Makofi)*

(b) Ni kwamba ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya yetu ya Tandahimba imejitahidi kujenga shule kwa nguvu za wananchi na tumeiomba Serikali izichukue shule zile. Ni shule 3 tu ya Mahuta, Tandahimba na Luagala. Lakini pamoja na uchache huo wa shule za sekondari tuna tatizo kubwa la walimu. Sasa nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri katika hali hii tuliyonayo anafanya utaratibu gani kututatulia tatizo hili la walimu kwenye shule hizi hizi tatu nilizozitaja?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru kwanza Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kwa kupongeza jibu letu na mimi napenda nimshukuru jibu lilikuwa hivyo kwa sababu swali lenyewe liliulizwa kwa ufasaha sana, ikabidi na majibu tujitahidi yawe kwa ufasaha vile vile.

Kuhusu maswali yake mawili ya nyongeza. La kwanza, tunafanyaje kuhusu uwiano usio sawa wa hivi sasa ambao umejitokeza katika maelezo niliyoyatoa.

Napenda nimhakikishie kwamba katika kuandaa Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari tumezingatia tofauti zilizopo. Kwa sababu ni sehemu ya kazi na wajibu wa bajeti ya Serikali kutumika kurekebisha kasoro zilizomo katika jamii.

Kwa hiyo, msingi unaotumika katika Mpango wa Maendeleo ya Sekondari ni kuhakikisha kwamba lile lengo tunalotaka kulifikia Kitaifa la kupeleka Sekondari asilimia 50 ya watahiniwa wa darasa la saba au rika lengwa kigezo hicho hicho tunajaribu kukifikia katika kila Wilaya.

Napenda nimfahamishe kwamba katika mpango huo siyo tu kupanua shule za sekondari zilizopo bali ni kujenga pia sekondari mpya zipatazo 1,500 ili tufikie kuwa na shule za sekondari zaidi ya 2,500 katika nchi yetu, tukitambua kwamba jirani zetu wa Kenya wana shule za sekondari 3,300 hivi sasa. Kwa hiyo, katika mpango huo ni kujenga pia shule za sekondari mpya. *(Makofi)*

Sasa kuhusu swali la pili, kwanza napenda nipongeze juhudi ambayo imeanza kufanywa katika Wilaya ambazo huko nyuma zilikuwa zinaonekana kama zinapiga usingizi katika suala hili la elimu. Lakini sasa hivi nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili akiwemo Mheshimiwa Abdula Lutavi, ambao wamejenga shule mpya za sekondari 3. *(Makofi)*

Kuhusu tatizo la walimu napenda nilihakikishie Bunge kwamba katika mpango huo wa *SEDP* yametazamwa mahitaji yote. Kwa hiyo, kuna *component* ya mafunzo ya walimu kama vile tulivyofanya kwenye *PEDP* hali ya walimu katika shule za msingi imeanza kubadilika. Hivyo hivyo katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari tumezingatia suala la mafunzo ya walimu kwa ajili ya shule za sekondari hizi ili wawepo walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Na. 42

**Miswada Kuandikwa kwa Kiingereza**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ibara ya 67(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweka sharti la kujua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza kuwa ni moja ya sifa ya mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge; na kwa kuwa lugha inayotumika ni Kiswahili au Kiingereza na siyo lugha zote mbili:-

(a) Kwa nini Miswada inayowasilishwa Bungeni inaandikwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa madhumuni na sababu tu?

(b) Kwa kuwa mijadala yote inakuwa kwa lugha ya Kiswahili; je, kwa nini Miswada yote isiandikwe na kupitishwa kwa lugha ya Kiswahili tu ili kutoa changamoto ya kukijenga na kukienzi Kiswahili?

(c) Kwa kuwa Miswada hiyo inayopitishwa kuwa sheria kwa lugha ya Kiingereza hutumika mpaka Mahakama za Mwanzo, ambazo kulingana na Sheria ya Mahakimu na Mahakama ya mwaka 1984 *(Magistrate's Court Act, 1984)* lugha ya Mahakama ya Mwanzo ni Kiswahili; je, Serikali haioni kwamba Miswada yote iwe inaandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuwatendea haki Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na raia ambao wengi hawajui lugha ya Kiingereza?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Miswada inayowasilishwa Bungeni inaandikwa kwa Kiingereza kwa sababu Tanzania inafuata mfumo wa sheria unaotumiwa na Wanachama wa Jumuiya ya Madola. Kwa sababu hiyo lugha inayotumika katika nyanja za mawasiliano ya kikazi, utoaji elimu, kibiashara na mahusiano ya kijamii. Hapa nchini kwetu hatua hii inarahisisha mawasiliano kwa watu wasiokijua Kiswahili na tukitambua kwamba hizi ni zama za utandawazi na mahusiano ya Kimataifa.

(b) Miswada bado itaendelea kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kujadiliwa kwa lugha yoyote kati ya Kiswahili au Kiingereza kama ilivyoelezwa na Kanuni ya 118 ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003. Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele katika kuandika, kutunga na kutafsiri sheria zinazogusa moja kwa moja maslahi ya wananchi ambao hawafahamu Kiingereza. Mfano wa Sheria hizo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Kanuni za Sheria za Mila za mwaka 1963 *(G.N.No.436/1963)* na Sheria ya Hati Miliki ya mwaka 1999.

Wizara yangu katika mpango wake wa muda mrefu inakusudia kuimarisha Kitengo cha *Legal Translation* ili Sheria ziweze kutungwa katika lugha zote mbili.

(c) Ni kweli kwamba sheria zilizotungwa na Bunge hutumika mpaka Mahakama za Mwanzo ambako lugha yake ni Kiswahili. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanajua Kiingereza na wamepewa mafunzo maalum kuhusu jinsi ya kutafsiri na kuzitumia sheria kwa maslahi ya wananchi. Pia hupewa mafunzo yanayowawezesha kutoa mwongozo kwa Wazee wa Baraza na Mashahidi wanapokuwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo naamini kwamba haki itatendeka kwa upande wa Mahakimu na wananchi kadhalika.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize kama ifuatavyo:-

(a) Je, kwa kutumia Kiingereza katika Sheria ambazo zinawahusu watu wa kawaida hatuoni kwamba tunakiuka haki za msingi kabisa za binadamu zinazotaka watu wazifahamu sheria ili waweze kuepuka makosa?

(b) Kwa kutumia lugha ya Kiingereza katika Bunge lako Tukufu hatuoni kwamba Serikali inaonyesha mfano mbaya ambao unavifanya hata Vyuo Vikuu viache kufundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, matumizi ya lugha ya Kiingereza ndani ya Bunge na katika Serikali yetu utaratibu huo kwa kweli haukiuki kabisa haki za binadamu. Katika Katiba yetu lugha zote hizi mbili zimetamkwa rasmi kwamba ndiyo lugha rasmi ambazo zitatumika katika Bunge hili na katika kuendesha shughuli zetu za Kiserikali. Kwa hiyo, kusema kwamba tunakiuka haki za binadamu si sahihi.

Suala la mahusiano baina ya Bunge hili kutumia Kiingereza na Vyuo vyetu Vikuu kukatishwa tamaa kutumia Kiswahili nalo si sahihi hata kidogo. Kwa sababu Kiingereza ni lazima kwa kweli tukipe mkazo unaostahili na hasa kwa wakati huu wa utandawazi. Nadhani hilo linatosha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Linatosha. Ili kuyapa nafasi maswali yote matatu yaliyobaki yajibiwe naomba kusiwe na maswali ya nyongeza.

Na. 43

**Sheria Kuzingatia Matunzo ya Mama na Mtoto**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi suala la watoto wanaozaliwa nje ya ndoa linapozungumzwa hujali tu watoto hao na sio mama zao ambao ama kwa kuzaa watoto hao wameshindwa kabisa kuolewa tena hivyo kuendelea kupata matunzo haba kwa mtoto peke yake; je, Serikali itakapokuwa inapitia sheria inayohusika itazingatia matunzo ya mtoto na mama kwa pamoja?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria, imefanya utafiti yakinifu kubainisha upungufu uliomo katika Sheria mbalimbali zinazowagusa watoto na wanawake ikiwemo Sheria ya Watoto, Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi.

Baada ya kubainisha upungufu katika Sheria, Tume iliyawasilisha mapendekezo hayo Serikalini. Wizara yangu ilikwishawasilisha Waraka Serikalini kwa kila Sheria.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali ni kwamba iandaliwe *White Paper* kwa ajili ya kupata maoni zaidi ya wananchi kuhusu marekebisho ya Sheria hizo. Majadiliano juu ya marekebisho ya sheria hizo yatakapokamilika Muswada utaandaliwa kwa ajili ya kuletwa Bungeni kujadiliwa kabla ya kupitishwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko katika sheria zinazohusu matunzo yatalenga zaidi watoto, kwa kuwa wao hawana kosa lolote juu ya utaratibu wa kuzaliwa kwao na hawana uwezo wa kujikimu kimaisha kutokana na hali yao ya utoto.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho katika sheria hizo hayakuwalenga akinamama kwa kuwa inatarajiwa kuwa mama hao watakuwa wanaelewa athari za kupata watoto hao nje ya ndoa. Akinamama wanatarajiwa kuwa waangalifu na wabahili kweli kweli wanapoingia katika mapatano ya namna hiyo. Ni vema akinamama wakaelewa athari za maamuzi yao badala ya kujiingiza kichwa kichwa katika suala zito kama hili. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nadhani mlisikia kauli eeh?

Na. 44

**Uvuvi wa kutumia Meli kubwa**

**MHE. KARIM SAID OTHMAN** aliuliza:-

(a) Je, tangu Sheria ya *The Deep Sea Fishing* ipitishwe na kuanza kazi, ni meli ngapi zimepatiwa leseni za kuvua samaki katika maeneo husika hadi leo?

(b) Je, Serikali inatumia mbinu gani kuhakikisha kwamba meli zilizopewa leseni ndizo zinazovua na je, mapato tunayopata yanalingana na mavuno yanayopatikana au kuwepo na utoroshaji wa aina fulani?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana tangu mradi huo uanze hadi wakati swali hili linapojibiwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu sheria hiyo ipitishwe hadi sasa jumla ya meli 193 zimepewa leseni za uvuvi kwenye Bahari Kuu. Kati ya meli hizo 64 zilipewa leseni upande wa Tanzania Bara ambapo meli 129 zilipewa leseni upande wa Tanzania Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, mipaka ya Ukanda wa Uchumi ya nchi inaendelea hadi umbali wa maili 200 *(200 nautical miles)* kutoka ufukweni. Umbali huo ni mrefu sana ukilinganishwa na uwezo wa Serikali kufanya doria za mara kwa mara kwenye eneo hilo kwa lengo la kudhibiti uvuvi bila leseni *(poaching).* Kwa hali hiyo ni vigumu kuhakikisha kuwa meli zilizopewa leseni ndizo zinazovua. Hata hivyo wenye meli zisizopewa leseni hutoa taarifa wanapoona meli zinapora samaki katika eneo hilo.

Aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kupitia Mkataba wa *SADC* wa kusimamia shughuli za uvuvi kuna mradi wa ushirikiano wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo katika udhibiti wa uvuvi kwenye maji chumvi *(SADC Fisheries Monitoring Control Surveillance Programme).*

Mheshimiwa Spika, mapato yanayoingia Serikalini kutokana na uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi ni ada za leseni za uvuvi pamoja na ya kuandikisha vyombo vya uvuvi. Kwa kuzingatia hilo hakuna utoroshaji wa aina yoyote wa mapato ya Serikali kwani ada za leseni hizo hulipwa kabla meli hazijaanza kuvua.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichopatikana tangu utoaji wa leseni za uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi uanze hadi Septemba, 2003 ni shilingi 982,895,985.60 kutokana na leseni zilizotolewa upande wa Tanzania Bara na shilingi 242,340,000/= upande wa Tanzania Zanzibar.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Namshukuru Mheshimiwa Kapteni Theodos Kasapira, mwenye swali linalofuata ameomba lipangiwe muda mwingine kwa kuona kwamba muda wa maswali wa leo umekwisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine Waheshimiwa Wabunge. Lakini kama kawaida kabla ya hapo kuna matangazo.

La kwanza nilieleza jana lakini nikumbushe kwamba baada ya kipindi hiki cha maswali, tutakuwa na semina ambayo imeandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na ratiba yake tumeshaigawa isipokuwa pale inaposema kutakuwa na kujiandikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge watapata chai na baadaye kujiandikisha. Hakuna sababu ya kujiandikisha kwa sababu yale mambo ambayo yanaambatana na semina tutatumia orodha ya mahudhurio ambayo mmeshaisaini tayari. Hakuna haja ya kujiandikisha upya. *(Makofi)*

Sasa vikao vya Kamati, Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Kamati yake ikutane kufikiria Azimio tulilowapelekea la *Optional of Protocol to the Convention on the Elimination of all Forms of Discrimination Against Women.* Kamati ikutane katika vyumba vya Kamati huko. Hakutaja muda lakini naamini itakuwa ni baada ya kipindi hiki cha maswali, lakini kuna semina nyingine. Sasa nadhani Mwenyekiti utakubaliana na Kamati yako lini mkutane.

Kikao cha Wabunge Wanawake *(TWPG)* wanakutana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Tafadhali Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge Wanawake pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii wakutane leo tarehe 5 Februari, 2004 mara baada ya semina kutakuwa na kikao kitakachofanyika Chumba namba 231. Mara baada ya semina ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ndiyo anathibitisha. Kumbe vikao vyote viwili Wabunge Wanawake na Kamati ya Maendeleo ya Jamii itakaa baada ya semina kumalizika, semina ya Wizara ya Biashara na Viwanda.

Tangazo la mwisho, naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna nafasi mbili zimetokea katika Wabunge wanaochaguliwa na Bunge hili kwenda katika vyombo mbalimbali. Nafasi ya kwanza imetokea katika Wajumbe wetu wanaokwenda *SADC Parliamentary Forum.* Nafasi ya wazi imetokea kwa sababu Mheshimiwa Anne Makinda, aliyekuwa anawakilisha kundi la Wanawake katika

*SADC Parliamentary Forum* amejiuzulu. Ameleta barua ya kujiuzulu kwa hiyo, nafasi sasa iko wazi. *(Makofi)*

Nafasi ya pili ambayo iko wazi ni ya Tume ya Huduma za Bunge kwa kundi la Kambi ya Upinzani. Kundi hilo lilikuwa linawakilishwa katika Tume ya Huduma za Bunge na Mheshimiwa Danhi Makanga. Sasa Ubunge wake ulipokoma basi na nafasi ikawa wazi, ni vizuri ikajazwa na Mbunge mwingine kutoka Kambi ya Upinzani.

Sasa kanuni inayotuongoza katika hilo inasema kama ifuatavyo: "Kwamba ikitokea nafasi ya namna hiyo, Spika atatoa taarifa ya kutokea kwa nafasi hizo kwa Wabunge wote Bungeni" na ndiyo kazi ninayoifanya sasa.

Baada ya hapo kama ni nafasi za makundi ama ya Wanawake au ya Upinzani: "Mbunge yeyote wa kundi linalohusika anayetaka kuwa mgombea wa nafasi hiyo atawasilisha jina lake kwa Katibu wa Bunge angalau siku moja kabla ya siku ya uteuzi atakayokuwa ameiweka. Sasa nimearifiwa na Katibu wa Bunge angependa uchaguzi tuufanye siku ya Jumatatu ijayo.

Kwa hiyo, ameweka siku ya mwisho ya uteuzi iwe ni kesho Ijumaa saa za mwisho za Shughuli za Bunge, hapo Bunge linapomaliza shughuli zake awe amepokea maombi yote ya wale wanaotaka kushiriki kutoka katika Makundi haya mawili.

Lakini nielezee zaidi kwamba kila Bunge linajijengea utamaduni wake. Sasa katika utamaduni wetu wa uchaguzi ndani ya Bunge nafikiri ingefaa tujiwekee utamaduni ufuatao kwamba Bunge ni chombo cha demokrasia, kwa hiyo, uchaguzi unaofanywa na Wabunge ndani ya ukumbi huu ni lazima uwe wa kidemokrasia.

Kwa hiyo, ni vizuri Makundi haya yatoe nafasi kwa kila anayetaka kugombea agombee, kundi lisituletee msimamo wa mgombea mmoja kwamba sisi kundi letu linamtaka fulani, hapana. Kila Mbunge ana haki ya kugombea na wapiga kura hao hawataki kuletewa jina moja ili wapige muhuri, si vizuri.

Kwa hiyo, tupanue *Electoral Democracy* yetu iwe wazi kwa kila mtu anayetaka, kusiwe na misimamo, kwa Kambi ya Wanawake tuletewe wote wanaotaka kugombea, kwa Kambi ya Upinzani tuletewe wote wanaotaka kugombea, Wabunge watapiga kura kuchagua yule wanayemtaka. *(Makofi)*

Basi baada ya maelezo hayo sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. Sasa hivi tufanye semina saa 11.00 jioni ndiyo Mheshimiwa Waziri atawasilisha Muswada ili usomwe mara ya pili.

*(Saa 04.41 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Kukabiliana na Bidhaa Kutoka kwa Wazalishaji wa Nje Wenye Nia ya Kuua Ushindani wa Ndani wa Mwaka 2003 *(The Anti-Dumping and Countervailing Measures Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya kujihami na bidhaa kutoka Nje zinazouzwa bei ya chini kwa makusudi ili kujipatia soko na hatua za kuzuia na kufidia athari zake *(Anti-Dumping and Countervailing Measures Bill, 2003)* sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza na kuishukuru kwa dhati kabisa, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa kuuchambua kwa undani na kwa kina Muswada huu na hatimaye kuishauri Serikali namna ya kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru vile vile Waheshimiwa Wabunge, ambao walitupatia michango yao ambayo imetuwezesha kupata mwanga zaidi katika kuandaa Muswada wa Sheria ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures* unaopendekezwa kwa mara ya kwanza hapa nchini. Kama mnavyofahamu, kwa muda mrefu sasa yamekuwepo malalamiko ndani ya nchi na jamii yetu miongoni mwa Wawekezaji wa Sekta ya Viwanda na hata miongoni mwa Wananchi wa kawaida kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua kamambe za kulinda viwanda vyetu dhidi ya ushindani usio wa haki kutokana na bidhaa zinazoingizwa nchini. Zipo dalili zinazoonyesha kuwa baadhi ya viwanda vyetu vya nguo, matairi, viberiti na kadhalika, vinaathiriwa na tatizo hilo. Katika miaka iliyopita Taifa limekuwa likichukua hatua za Kitaifa katika kukabiliana na tatizo hili kwa kutumia nyenzo zifuatazo: -

(i) Kiwango cha chini cha ushuru *(Minimum Dutiable Value);*

(ii) Kutoza ushuru wa ziada juu ya ushuru wa kawaida *(Suspended Duty);* na

(iii) Ukaguzi wa ubora wa bidhaa kutoka nje.

Licha ya hatua hizi, tumefikia mahali ambapo Taifa la Tanzania kama sehemu ya Jumuiya ya uchumi ya Kimataifa ambayo ni Mwanachama wa Shirika la Biashara Ulimwenguni *(World Trade Organisation - WTO),* linapaswa kuzingatia na kutekeleza makubaliano yanayotokana na mikataba ya kibiashara ya Shirika hili. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, muda wa masharti nafuu ambayo tulipewa kama nchi changa unakaribia ukingoni na inabidi kuanza maandalizi kamambe ya kutimiza wajibu na kupata faida zinazotokana na uanachama wetu katika chombo hiki.

Mojawapo ya maeneo muhimu katika mfumo huu unahusu suala la athari kwa viwanda vya nchi wanachama unaotokana na ushindani usio wa haki kutokana na bidhaa za nchi nyingine zinazouzwa kwa bei iliyo chini ya gharama za uzalishaji wake katika nchi zinazotoka. Ingawa Sheria ya *Anti-Dumping* inatumika sana katika nchi zilizoendelea, nchi zinazoendelea zimeanza kuongeza kasi ya kutumia nyenzo hii. Uwezekano wa Tanzania kuitumia unapaswa kwanza kwa kutunga sheria ya aina hii na kuelimishana kuhusu matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utatuwezesha kutungwa kwa sheria ambayo inalenga kuwalinda wawekezaji, viwanda vilivyopo na walaji dhidi ya baadhi ya wazalishaji na wasambazaji ambao baada ya kuua ushindani kwenye soko kwa kutumia ruzuku au upunguzaji wa bei makusudi, hupandisha bei ya bidhaa hizo maradufu kufidia hasara zilizopatikana huko nyuma. Sheria hii ni moja ya sheria muhimu katika uchumi wa soko ambayo inawezesha kusimamia uchumi wa soko kwa misingi ya sheria na uwazi kwa wahusika wote. Kwa hiyo, sheria hii ikisimamiwa vizuri na kwa dhati, huongeza imani kwa Wananchi na Wawekezaji katika uchumi wa nchi husika. Kuungwa mkono kwa sheria hii na kuiwezesha kufanya kazi ipasavyo ndiyo njia muhimu ya kuhakikisha kuwa faida zinazotokana na uchumi wa soko zinagusa sehemu kubwa zaidi ya jamii yetu kuliko kuwaachia wazalishaji wachache wa nje kutumia vibaya uchumi wa soko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu kumi na tatu. Sehemu ya kwanza, inaeleza mambo ya kiutangulizi ikiwa ni pamoja na jina fupi la sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na tafsiri ya baadhi ya maneno maalum yanayotumika katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, imeunda Kamati ya Ushauri *(Advisory Committee)*. Kazi na uwezo wa Kamati hii umeelezwa katika sehemu hii. Kamati hii ndiyo chombo pekee kitakachokuwa kinamshauri Waziri kuhusu punguzo la makusudi la bei ya bidhaa na uwekaji wa ruzuku kwenye bei za bidhaa husika. Katika sheria hii, Waziri wa Viwanda na Biashara, ndiye atakayekuwa anapokea malalamiko kutoka kwa wazalishaji na wanunuzi wa bidhaa na kuyapeleka kwenye Kamati hii

kwa ushauri. Kamati pia itahusika na masuala ya uchunguzi kama Waziri atashauriwa na kuridhika kuwa kunahitajika kufanyika uchunguzi huo *(investigations).*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, inaeleza namna ya kuzitambua bidhaa zilizopunguzwa bei makusudi au kuwekewa ruzuku hivyo kusababisha ushindani usio wa halali katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada, imeeleza namna ya kubaini athari kwa viwanda vyetu zinazosababishwa na bidhaa zenye punguzo la makusudi la bei au zilizopewa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano, inatoa taratibu za namna ya kufanya uchunguzi kwa ajili ya kuthibitisha kuwepo kwa bidhaa ambazo ama kwa makusudi zimepunguzwa bei au zimepewa ruzuku. Sehemu hii pia inaelezea kuwa malalamiko yote apelekewe Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita, inatoa masharti kwamba, taarifa zote ziwe na ushahidi *(evidence)* kabla ya kuridhika na kuamua kuwa hatua zichukuliwe kwa bidhaa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba, inampa uwezo Waziri wa kuchukua hatua za kisheria hata kabla ya utafiti kukamilika kama ataona kuwa kuna athari kubwa kwa viwanda vyetu inayoletwa na bidhaa husika kiasi kwamba athari hiyo ikiachwa ikatokea itakuwa vigumu kukifidia kiwanda husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, inampa Waziri uwezo wa kusitisha au kusimamisha kuchukuliwa hatua za kisheria kama mzalishaji baada ya kusikia malalamiko kuhusu athari inayoletwa na bidhaa zake kwa hiari yake mwenyewe akarekebisha bei ya bidhaa zake kwa kiasi ambacho Kamati itaridhika kwamba, marekebisho hayo yatapunguza au kuondoa athari inayoletwa na punguzo la makusudi la bei au uwekaji wa ruzuku.

Sehemu ya tisa, imeelekeza namna ya kutoza na kukusanya ushuru unaotokana na adhabu ya kosa la kupunguza kwa makusudi bei ya bidhaa au kuweka ruzuku kwenye bei ya bidhaa. Adhabu hiyo itatolewa tu baada ya kuridhika kupitia uchunguzi na ushahidi uliotolewa kuwa bidhaa hizo kweli kwa makusudi zimepunguzwa bei au kuwekewa ruzuku.

Sehemu ya kumi, inafafanua mazingira ambayo yatasababisha kuzichukulia hatua za kisheria bidhaa ambazo kwa makusudi zimepunguzwa bei au kupewa ruzuku.

Sehemu ya kumi na moja, imetoa muda wa kufanya marejeo *(review)* ya ushuru unaotozwa kama adhabu kwa bidhaa zinazoingia nchini ambazo zinasadikiwa kuwa zimepewa ruzuku au kwa makusudi zimepunguwa bei.

Sehemu ya kumi na mbili, inaipa Kamati uwezo wa kuzitangaza kwa umma bidhaa ambazo Kamati imeridhika kuwa zinastahili kupewa adhabu ya kuongezewa ushuru.

Sehemu ya kumi na tatu na ya mwisho, inaelezea maeneo matatu tofauti, yaani malalamiko kutoka nje ya nchi na taratibu za kuyashughulikia, makosa na adhabu mbalimbali na mwisho, madaraka aliyopewa Waziri ya kutunga kanuni namna ya kutatua migogoro.

Mlalamikaji kutoka nje ya nchi yetu akilalamikia bidhaa pia kutoka nchi nyingine ambazo zinaharibu soko la bidhaa zake katika nchi yetu ana haki ya kusikilizwa. Malalamiko hayo yataiomba nchi yetu itumie sheria hii kwa bidhaa zinazolalamikiwa. Hata hivyo, sehemu hii inamtaka mlalamikaji wa namna hii alete ushahidi wa kutosha kuhusu bei na athari zinazopatikana kwa kiwanda chake kutoka nchini kwake. Pia, sehemu hii inamtaka mlalamikaji wa namna hiyo atoe msaada utakaohitajika ili kupata taarifa za ziada ambazo Kamati inahitaji. Aidha, makosa na adhabu ni zile zitakazotolewa kwa yeyote atakayetoa taarifa za uongo, atakayetangaza taarifa za siri zilizotolewa wakati wa uchunguzi bila ya ruhusa na atakayekataa kutoa taarifa zinazotakiwa na Kamati bila sababu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa sheria yoyote ile haupo katika lugha ama vipengele vya sheria yenyewe, bali katika utekelezaji wake. Kwa maana hiyo, kuwa na sheria nzuri inayokidhi matakwa

ya jamii kwa wakati husika ni hatua moja tu, bado ni muhimu kuwa na Wananchi kwa ujumla na hususan wadau mbalimbali ndani ya jamii wanaoifahamu sheria hiyo pamoja na wajibu na haki zao ndani ya sheria husika. Ingawa Serikali ina uwezo wa kutunga sheria kupitia Bunge, inayokidhi matakwa ya Wananchi, bado jukumu kubwa la utekelezaji wake lipo mikononi mwa Wananchi wenyewe kwa kushirikiana na Serikali yao. Ukweli huu upo pia kwa Muswada tunaozungumzia leo hii. Serikali inaweza kuchukua hatua kadhaa katika kutekeleza sheria itakayotokana na Muswada huu, lakini jukumu ambalo litaiwezesha Serikali kuchukua hatua hizo kimsingi lipo zaidi kwa wadau ambao wanaathirika na mwenendo unaosababisha vitendo vya *dumping.*

Ufanisi halisi wa sheria hii utategemea sana umahiri wa Sekta Binafsi hususan wanaviwanda kutambua kuwepo kwa tabia ya *dumping*, kukusanya baadhi ya ushahidi utakaoiwezesha Serikali kufanya maamuzi ya awali ya kufanya uchunguzi wa kina na kushirikiana na Vyombo vya Serikali wakati wa uchunguzi huo. Hili ni eneo linalohitaji ushirikiano wa karibu wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, maoni ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara juu ya Muswada huu tumeyapokea na tumeyazingatia kama ilivyoonyeshwa kwenye marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. SALOME J. MBATIA (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kama hivi, ninaomba nami nitoe kheri ya mwaka mpya kwa Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikitakie Chama cha Mapinduzi kheri na pongezi nyingi sana kwa kutimiza miaka 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati ya Uwekezaji na Bashara kuhusu Muswada wa Kutunga Sheria ya Kujihami na bidhaa kutoka nje zinazouzwa bei ya chini kwa makusudi ili kujipatia soko na hatua za kuzuia na kufidia athari zake *(Anti-Dumping and Countervailing Measures Bill, 2003).*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Kutunga Sheria inayokabiliana na bidhaa kutoka kwa wazalishaji wa nje wenye nia ya kuua ushindani wa ndani *(Anti-Dumping and Countervailing Measures Bill, 2003).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutimiza masharti ya kanuni ya 70(2) toleo la mwaka 2003, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa umakini na ushirikiano wao wakati Kamati inafikiria Muswada wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 88 (6) na (69) toleo la mwaka 2003, Kamati yangu ilitoa mwaliko kwa wadau na Wananchi kwa ujumla, kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni na ushauri chini ya utaratibu wa *Public Hearing* ili kuboresha Muswada wa sheria hii kabla ya kufikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwashukuru na kuwatambua wadau hao kama ifuatavyo: Shirika la wenye Viwanda Tanzania *(CTI),* Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, *Aluminium Africa (ALAF)*,

*Bakhresa Group of Companies, Tanzania Brush Products Limited, Ulanga West Development Association, Intercont Tanzania Limited* na Vyombo mbalimbali vya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kualika wadau kufika mbele ya Kamati zinazokuwa zinachambua Miswada ya Sheria siyo tu unarahisisha kazi ya kufikiria Muswada wa Sheria husika, bali pia unawapa wadau na Wananchi kwa ujumla, fursa ya kushiriki katika mchakato wa kutunga sheria na hivyo kuepusha haja ya Bunge lako Tukufu kuzifanyia marekebisho ya mara kwa mara sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2003, sasa ninaomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Kutunga Sheria itakayokabiliana na bidhaa kutoka kwa wazalishaji wa nje wenye nia ya kuua ushindani wa ndani *(Anti-Dumping and Countervailing Measures).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Serikali ya kuleta Muswada wa Sheria hii wenye lengo la kuweka utaratibu wa kisheria wa kukabiliana na tatizo la uingizaji nchini bidhaa ambazo zina ubora wa viwango vinavyotakiwa, lakini vimepunguzwa bei kwa makusudi au zimepata ruzuku na hivyo kuzifanya bidhaa za viwanda vyetu kukosa soko la ndani kwa kushindwa kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa maoni na ushauri kuwa kifungu cha 5(1) katika sehemu ya pili, kinachounda Kamati ya Ushauri *(Anti-Dumping and Countervailing Measures Committee - ACMC),* kifanyiwe marekebisho ili angalau Wajumbe wawili wa Kamati hiyo watoke kwenye Sekta Binafsi. Aidha, kati ya Wajumbe hao wawili mmoja ni vizuri sana awe mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa Sekta Binafsi hivi sasa ndiyo mhimili na *engine* ya maendeleo ya uchumi wa Tanzania katika mazingira ya utandawazi, hivyo kushiriki kwao kwenye Kamati hii kuna umuhimu wa kipekee. Kamati ya Uchunguzi ipewe uwezo wa kutosha kisheria wa kupata habari na nyaraka mbalimbali ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inaunga mkono hoja ya kuanzisha Kamati Ndogo ili kusaidia Kamati ya Ushauri na hivyo kuleta ufanisi kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 6(2)(ii). Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa kazi na majukumu ya Kamati Ndogo nayo yaainishwe kama ilivyo kwenye Kamati ya Ushauri. Uainishaji huu unaweza kuwekwa katika Kanuni ambazo Waziri atazitunga kwa mujibu wa kifungu cha 77 sehemu ya kumi na tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 31(5) cha Muswada, kinaainisha muda wa ukomo wa uchunguzi wa bidhaa zinazoshukiwa kuingizwa nchini na kuuzwa kwa bei ya chini kuwa ni miezi 12 hadi miezi 18. Pamoja na ugumu wa kupata ushahidi, Kamati ina maoni na ushauri kuwa, muda huo ni mrefu na unaweza kusababisha athari zaidi kwenye bidhaa na uzalishaji kwenye viwanda kwa jumla. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kwamba, muda huo uangaliwe upya ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya *Anti-Dumping* ni ngeni miongoni mwa wenye viwanda na Wananchi kwa ujumla. Aidha, dhana hii mara nyingi huhusishwa na ubora wa bidhaa, tafsiri ambayo si sahihi. *Dumping* pia hutafsiriwa katika Kiswahili kama dampo la taka na hivyo dhana nzima ya *Anti-Dumping* kutafsiriwa kama ni uingizaji wa bidhaa kutoka nje zenye ubora hafifu au zilizokwisha muda wake wa matumizi. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha na kuwaelimisha wadau mbalimbali hususan wenye viwanda na Wananchi kwa ujumla ili sheria iliyotungwa iweze kutekelezeka bila kupoteza shabaha yake. Bila kutoa elimu ya kuhamasisha wenye viwanda na Wananchi kwa ujumla, kazi ya kuanzisha uchunguzi wa kuwepo *dumping* kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 27(1)(v), itakuwa vigumu kutekeleza sheria hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya sababu zinazofanya bidhaa za viwanda vya Tanzania kushindwa kushindana na bidhaa kutoka nje ya nchi ni gharama kubwa ya uzalishaji inayosababishwa na bei kubwa ya umeme, maji na mawasiliano. Hivyo, pamoja na kutunga Sheria ya Kujihami na bidhaa kutoka nje kuuzwa kwa bei ya chini kwa makusudi, Kamati inaishauri Serikali kwamba, ichukue hatua ya kupunguza gharama hizo ili kuongeza ushindani wa bidhaa zetu kwenye soko la ndani na la nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano wake wa karibu na Kamati yangu kila ilipokuwa inatekeleza kazi zake zinazohusu Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, nawashukuru pia Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ahmada Ngemera, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati yangu. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa wakati wa vikao vya Kamati. Napenda kuwaweka katika kumbukumbu kama ifuatavyo: Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Omari S. Chubi, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga na Mheshimiwa Aisha P. Magina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha na Mheshimiwa Christopher S. Wegga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Daniel Eliufoo, kwa kuihudumia Kamati hii ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (k.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami niwatakie *Happy Birthday* ndugu zangu wa CCM, kwa kuendeleza na kudumisha amani katika nchi wakishirikiana na Vyama vya Upinzani vilivyoko Tanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe ya leo kwangu mimi ni muhimu sana, ndiyo siku niliyochaguliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na tarehe 6 nikaapishwa mwaka 1982. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba vile vile niwatakie kheri ya mwaka mpya Waheshimiwa Wabunge wote, *Inshallah* Mwenyezi Mungu atujaalie matatizo yetu ya ukame na mengine yaondoke ili Taifa letu lizidi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo kwa niaba ya Mheshimiwa Mbowe, Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa *Anti-Dumping and Countervailing Measures, 2003* kama ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na wapigakura wote, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa kutunga Sheria itakayokabiliana na bidhaa kutoka kwa wazalishaji wa nje yenye nia ya kuua ushindani wa biashara ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa Muswada huu ni muhimu sana hususan katika nchi yetu ambao uchumi wake bado ni mchanga sana ambao unahitaji kila aina ya ulinzi ili uweze kukua. Hii haina ubishi kuwa Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka kabisa hasa ukilinganisha na kipindi hiki kilichojaa kila aina ya udanganyifu kwenye biashara. Udanganyifu huu waweza kuwa wa ndani ya nchi au

wa nchi moja kuihujumu nchi nyingine na hasa kwa kutoa ruzuku kwa bidhaa zinazoletwa hapa ili kuua bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Kwa ujumla, *dumping* ipo ya kutosha hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sheria itatekelezwa ipasavyo, itachochea ushindani wa kweli na haki katika biashara za bidhaa za viwanda vyetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mheshimiwa Waziri kutamka bayana kuwa Muswada huu ni maalum kwa ajili ya viwanda, lakini amesahau kuwa viwanda haviwezi kuwepo bila ya kuwa na malighafi za viwanda hivyo. Viwanda vingi malighafi zake zinatoka kwenye Sekta nyingine zaidi ya viwanda. Hivyo basi, bila kulinda malighafi zinazozalishwa hapa kwetu bado hatujalinda viwanda vyetu na hatuwezi kuwa washindani wa kweli kwenye soko la ndani na nje.

Ushauri wetu kwa Waziri ni kulinda vyanzo vya ndani vya malighafi ambazo nyingi zake ni za kilimo. Kwa mfano, uliotolewa hapa asubuhi shayiri leo inaagizwa kutoka *South Africa* wakati shayiri inayolimwa Tanzania na Watanzania wenyewe, wakulima hawana soko la kuuza. Hiyo ni malighafi ambayo kama haikulindwa wakulima hawa wataendelea kuwa maskini, wakulima hawa wataendelea kuwa ombaomba na *dumping* kwa aina nyingine itakuwa imetokea. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikakaa ikaliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni ngumu kutekelezeka kwa sababu dhana ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures* ni mpya nchini kwetu hususan kwa watu ambao ni watumiaji wa bidhaa za nje. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuendelea na kuchukua jukumu la kuwaelimisha Wananchi na wale watakaoitekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Kamati ya ushauri kama ilivyobainishwa kwenye ibara ya tano kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo, wengi watatoka Serikalini, ukiacha Mjumbe mmoja atakayetokea *CTI* na *TCCIA,* muundo wa Kamati hii umesahau sekta binafsi ambayo ndiyo inasimamia uzalishaji mali. Tunaishauri Serikali ihusishe sekta hiyo kwani ndiyo wanaozalisha bidhaa na itakuwa rahisi kudhibiti *dumping*. Pia nashauri Serikali itengeneze mkakati madhubuti wa sheria hii ili kuwepo na uwajibikaji kati ya Serikali, wazalishaji na wenye viwanda juu ya *dumping.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii isipingane na dhana nzima ya utandawazi ambapo Tanzania imeshafungua milango. Tumeshuhudia Tanzania ikijiunga na Jumuiya mbalimbali za kiuchumi na kisiasa kama vile *East African Community, SADC* na kesho kutwa tutaingia kwenye *NEPAD.* Jumuiya hizi zimekuwa zikihubiri soko huria, tunashauri Serikali kutoa motisha kwa ajili ya bidhaa za viwanda vyetu ili iweze kushindana kwa njia ya bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada haujalenga kulinda mali ghafi zinazopatikana hapa nchini, viwanda vingi vinatumia mali ghafi kutoka nje. Tunaishauri Serikali ifanye utafiti ili kuona ni viwanda vingapi vinatumia mali ghafi ya ndani, vingapi vinategemea mali ghafi kutoka nje. Kwa njia hiyo, tutaweza kujua jinsi ya kutoa motisha kwa wazalishaji wa ndani wa mali ghafi, kitu kitakachosaidia kuinua viwanda na kuwezesha ushindani mzuri kwenye masoko yetu yote ya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaunga mkono mia kwa mia Muswada huu na inaomba Waheshimiwa Wabunge, waupitishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ilikusudiwa Muswada huu ujadiliwe kesho baada ya maswali ili muweze kupata nafasi ya kupitiapitia haya yaliyosemwa na yale tuliyoyapata kwenye semina ili kesho tuwe na mchango mzuri zaidi.

Sasa leo asubuhi Mheshimiwa Spika, alitangaza kujiuzulu kwa Mheshimiwa Anne Makinda, katika ile nafasi yake ya Uwakilishi kwenye vikao vya *SADC,* lakini hapakutolewa maelezo ya kina. Kwa hiyo, Mheshimiwa Anne Makinda, ameomba apate nafasi ya kutoa maelezo ya kina. Kwa hiyo basi, kwa kutumia kifungu cha 21 cha Kanuni za Bunge, nitamwita Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, aweze kutoa hoja ya kuahirisha Bunge ili kumpatia nafasi ya kutoa maelezo. *(Makofi)*

**KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE**

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI ( k.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa Kanuni zetu kifungu cha 21(6), naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe kabla ya wakati wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, kama nilivyosema, kabla sijawahoji sasa namwita Mheshimiwa Anne Makinda, kwa ajili ya maelezo binafsi.

**HOJA YA KUJIUZULU UJUMBE WA *SADC PARLIAMENTARY FORUM***

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kutoa shukrani zangu kwa kupewa nafasi hii, niweze kujieleza kinagaubaga dhana yangu ya kuomba kujiuzulu Ujumbe katika *SADC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 40, naomba nitoe maelezo yangu binafsi.

Baada ya Katiba ya *SADC Parliamentary Forum* kufanyiwa marekebisho ambayo yalipendekezwa na Bunge letu na kuungwa mkono na Mabunge mengine ya nchi hizi za *SADC* kwamba sasa Uwakilishi wa Wabunge katika Bunge la *SADC* ni wa Wabunge Wanaume wawili na Wabunge Wanawake wawili, ukiacha nafasi ya Spika. Kati ya Wabunge hao Wanawake, mmoja atakuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa Bunge la Bunge husika. Ibara ya 6(3) ya Katiba iliyorekebishwa sasa inasomeka kama ifuatavyo: *"A SADC Parliamentary Forum shall consist of Presiding Officers and four Representatives elected by each National Parliament provided that in electing the four Representatives, each National Parliament shall:-*

*(a) Ensure equitable Representation of Women and Political Parties that are represented in the Parliament.*

*(b) Include the Member of the Executive Committee of the Regional Women Parliament caucus.*

Hii *Regional Women Parliamentary caucus* kwamba hii *TWPG* na zingine za Mabunge mengine, ndiyo zinazounda Chama cha Wanawake Wabunge wa *SADC*. Kwa hiyo, Wenyeviti wa Vyama vya Wanawake Wabunge wa nchi mbalimbali wanakuwa Wajumbe wa *SADC* moja kwa moja na *Umoja Executive Committee/ Steering Committee* ya ile Wanawake Wenyeviti wote pia ni Kamati mojawapo ya *SADC.* Kwa msingi huo wa mabadiliko hayo, mimi nipo katika nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wabunge katika Bunge letu yaani *TWPG.*

Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabungewote, kwa heshima kubwa mliyonipa mwaka 2001, kwa kunichagua kuwawakilisha katika Bunge la *SADC Parliamentary Forum*. Nikiwa kule kwa nafasi mliyonipa nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji *(Executive Committee)* ya *SADC,* nimewahi pia kuwa Mjumbe wa Kamati Ndogo ya Fedha ya Kamati ya Utendaji ya *SADC* na sasa nipo katika Kamati ya Utendaji *(Steering Committee)* ya Chama cha Wanawake Wabunge wa Kanda ya *SADC,* kwa nafasi hiyo ya kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa Bunge. *(Makofi)*

Hivyo, nafasi niliyopewa kwa kura za Waheshimiwa Wabunge humu ndani, naomba niirejeshe kwenu ili achaguliwe Mbunge Mwanamke mwingine kujaza nafasi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi bado ni Mjumbe wa *SADC* kwa kofia nyingine. Naahidi kuendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote katika mfumo mzima wa kuimarisha Bunge letu na Mabunge ya Kanda tunayoshirikiana nayo. Naomba ombi langu la kujiuzulu nafasi ya Uwakilishi ndani ya Bunge la *SADC* kupitia kura zenu likubaliwe na mnione nimewaheshimu nafasi yenu. Naomba tujenge Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtaona kwa nini Mheshimiwa Spika alikubali ajiuzulu, kwa sababu bado ataendelea kuwa Mjumbe wa kutuwakilisha kule *SADC.*

Baada ya maelezo hayo, sasa muiamue hoja ya kuahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kujiuzulu Ujumbe wa SADC Parliamentary Forum ilikubaliwa na Bunge .*

*(Saa 11.36 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 6 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*